

Mauzo ya mboga zilizokaushwa

Kilo moja ya mboga zilizokaushwa huhitaji kilo
7 za mboga mbichi. Hivyo: tani $4.6 \times 1000 =$
 $4600/7 =$ kilo 655

Baada ya kuvuna tani 4.6, mkulima anapata kilo
655 zilizokauka.

Kilo moja huuzwa shilingi 600.

Hivyo mkulima anapata
 $655 \times 600 =$ shilingi 393,000.

Kwa kuuza mboga za kukaushwa mkulima apata
ziada ya $(393,000 - 184,000) =$ shilingi 209,000.

Pesa hizo ziatagharamia ukaushaji na kazi
iliyofanywa.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Barua pepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Nasambu Okoko, Finyange Pole, C.K. Katama

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Mtwapa

S.L.P.16-80109 Mtwapa

au

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI – Kisii SLP 532 Kisii, 40200

Simu: 058 31800/1/2/3 au 058 31800

Barue: kari-kisii@westnet.co.ke

Kari_kisii@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 61 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Jinsi ya kuhifadhi mboga za kiasili za kutumia wakati wa kiangazi



Utangulizi

Mboga za kiasili ni muhimu kwa chakula na zina virutubishi zaidi ya zile za kigeni kama vile sukuma wiki na kabeji.

Mifano yake ni kama vile sageti, mnavu, mchicha na mkunde. Mimea hii huwa na madini na vitamini A zinazohitajika kwa afya ya binadamu.

Mazao ya tani 0.8 hadi 4.6 kwa kila hektari yanapatikana iwapo mbolea za FYM pamoja na DAP na CAN zinatumiwa pamoja.

Wakati wa mvua nyingi mazao huwa mengi na wakati wa kiangazi mazao hupungua. Namna rahisi kama kuweka kwa maji yaliyochemka hatimaye kukausha kwa miale ya jua huwezesha mboga hizi kuwekwa kwa muda mrefu.

Faida za kuhifadhi mboga

- Kuwa na chakula cha mboga kila wakati.
- Hutumia muda mfupi wa kupika na ladha yake ni kama ya kuvunwa upya.
- Hudumu kwa muda mrefu na yaweza kusafirishwa mbali.

Mahitaji

- Mboga zenye kuvunwa hapo kwa papo
- Mitungu safi
- Sufuria au nyungu 4 au 5
- Vichunjio
- Vijiko vikubwa
- Maji safi
- Chumvi
- Kaushio cha miale ya jua
- Mifuko ya plastiki yenye uwezo wa kujifunga
- Kihifadhia kikubwa.

Hatua

Kusafisha

- Vuna mboga na ukate mihimili.
- Ondoa matawi yaliyokauka na asilia zingine za kigeni kisha uoshe na upitishie kwenye maji.

Kuchemsha

- Wekelea maji kiasi fulani katika sufuria ili kuchemka.
- Kwa kila lita moja ya maji weka chumvi kijiko kimoja.
- Tumbukiza mboga kwenye maji hayo yanayochemka.
- Koroga kwa muda wa dakika 5 ili kuhakikisha kila sehemu ya mboga imefikwa na maji.

Kupoesha na kukausha

Poesha mboga na maji baridi

- Tandaza kwenye trei mistari miembamba.
- Ziache zikauke kwa siku 2-5 kulingana na hali ya anga.
- Zitoe mboga kwa jua baada ya kukauka na uweke mahali kavu na baridi kwa muda mrefu kabla ya kuanza kupakia.

Kupakia

- Weka mboga katika mifuko ya gramu 100 inayofungika.
- Iweke katika mifuko isiyotoa wala kuingisha hewa mahali penye baridi na kavu kwa minajili ya kuuza au kutumia baadaye.

Mboga zilizohifadhiwa hivi zinaweza kudumu kwa muda wa miezi 6.

Faida za kiuchumi

Mauzo ya mboga mbichi

Kutoka kwa ekari moja, tani 4.6 zinapatikana.

Kilo moja ya mboga huuzwa kwa shilingi 40.

Kutoka kwa tani 4.6 mkulima anapata (4.6x1000x40) shilingi 184,000 kutoka kwa mboga .